




**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA**



YAH: TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA KWA FUNDI MAGARI NAFASI (1).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba anatangaza nafasi ya kazi ya mkataba na anakaribisha maombi kwa watazania wenye sifa za kujaza nafasi kama ilivyoorodheshwa katika tangazo hili.

N.B: MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha nne na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. Viambatanisho hivyo vibanwe sawasawa kuondoa uwezekano wa kuondoka au kupotea. **(Passport size) ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.**
- v. Testimonials, "Provisional results", statement of results ", hati ya matokeo ya kidato cha Nne (FORM IV RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA.**
- vi. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- vii. **Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.**
- viii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **17/05/2022 saa 9.30 ALASIRI.**
- ix. Maombi yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kwa

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA
S.L.P 830
CHEMBA –DODOMA

MAJUKUMU YA KAZI.


- Kutengeneza na kusimamia wa magari na mitambo ya Halmashauri.
- Kufanya ukaguzi wa magari na mitambo ya Halmashauri ya Wilaya.
- Kuandaa taarifa na mahitaji ya ukarabati wa magari na matengenezo.
- Kuandaa makisio ya matengenezo ya magari na mitambo.

SIFA ZA MWOMBAJI.

- Awe na elimu ya kidato cha nne (Form IV)
- Awe na cheti cha kuhitimu mafunzo ya ufundi (Mitambo na Magari au Full Technician) kutoka katika cho kinachitambuliwa na Serikali.
- Mwenye cheti cha majaribio ya ufundi hatua ya I au II (Grade Taste I or II) kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Mwenye leseni ya udereva atapewa kipaumbele iwe daraja C.

MSHAHARA.

Tsh. (390,000/=) kwa mwezi.


**SIWEMA H. JUMAA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
CHEMBA.**